



## CHUO KIKUU CHA GARISSA

### MTIHANI WA MWISHO WA SEMISTA

Idara ya **Sanaa na Sayansi ya Kijamii**

Shahada ya **Elimu (B.Ed-Arts)**

Semista ya **Kwanza 2017/2018**

KIS 210: **Nadharia zaUhakiki wa Fasihi**

Muda: **Saa 3**

Tarehe: **14/12/2017**

Mkondo: **Regular**

**Maelekezo:** Jibu swali la **KWANZA** na maswali mengine **MATATU**

Swali la **KWANZA** ni la **LAZIMA**

- 
1. Ukitumia mifano mwafaka jibu maswali yafuatayo:
    - a) Jadili umuhimu wa nadharia za uhakiki wa fasihi kwa mtafiti [Alama 5]
    - b) Eleza shabaha zozote TANO zakuhakiki kazi za fasihi. [Alama 10]
    - c) Jadili vigezo vyovyoteVITANO vinavyotumiwa na wahakiki kubainisha nadharia bora ya uhakiki wa fasihi [Alama 10]
  2. Ukizingatia mihimili yoyote SABA ya nadharia ya ufeministi, eleza jinsi P. Jerono (2007) *Usaliti* anavyoshughulikia hali ya mwanamke katika jamii yake. [Alama 15]
  3. ‘Tamthilia ya E. Mbogo (2011) *Sundiata* inaakisi sifa za ulimbwende.’ Fafanua kauli hii ukitumia mifano yoyote SABA iliyo mwafaka kutoka katika tamthilia hiyo. [Alama 15]
  4. Fafanua kwa mifano dhahiri jinsi sifa zozote SABA za uhalisia wa kijamaa zinavyojitokeza katika riwaya ya H. Mwakyembe (2009) *Pepo ya Mabwege* . [Alama 15]
  5. Jadili madai MATANO kwa kila nadharia yanayopendekezwa na nadharia zifuatazo za uhakiki wa fasihi simulizi:
    - a) Nadharia ya Msambao [Alama 5]
    - b) Nadharia ya Uamilifu [Alama 5]
    - c) Nadharia ya Miundo na Maumbo Tengamano [Alama 5]
  6. Jadili sifa zozote SABA za urasimi mkongwe zinazojitokeza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulioko kwenye diwani ya M. Mulokozi (1999) *Tenzi Tatu za Kale*.

[Alama 15]